www.repoa.or.tz

Toleo Na 1/2019 Mei, 2019

Dokezo la Utafiti

# Mabadiliko ya Kitaasisi na Vikwazo vya Ushindani Kwenye Masoko: Tafiti Kuhusu Wakulima Wadogo Tanzania

*Na: Donald Mmari*

## Utangulizi

Historia ya sera nchini Tanzania imekuwa ni ya mabadiliko ya mara kwa mara ambayo lengo lake limekuwa ni kuongeza ufanisi na uzalishaji katika sekta muhimu za uchumi. Dokezo hili linatoa muhtasari wa kitabu kilichotokana na utafiti uliochunguza uwezo wa mabadiliko mbali mbali ya sera kuiongezea sekta ya kilimo, hususan wakulima wadogo, nguvu ya ushindani katika masoko mbali mbali ndani na nje ya Tanzania. Ushahidi utokanao na utafiti huu unaonyesha kwamba baadhi ya sera za kilimo zilizotungwa na kutekelezwa mara tu baada ya uhuru zilichangia kuzorotesha uzalishaji wa mazao ya biashara. Unaonyesha pia kwamba sera zilizolenga marekebisho ya kimuundo maarufu kama 'structural adjustment' na utandawazi hazikufanikiwa sana kuongeza uzalishaji kwenye kilimo kama ilivyotarajiwa. Kutokana na hilo hoja kubwa ni kwamba ili kuviondoa vikwazo hasi vya kisera kwenye mfumo wa soko vinavyopunguza ufanisi kwenye sekta ya wakulima wadogo, ni vizuri kutumia taratibu na mifumo ya kimasoko na isiyo ya kimasoko kwa uratibu mzuri wa pamoja.

### Upeo na kina cha utafiti

Utafiti ulitumia mbinu zitokanazo na fani mbali mbali za sayansi ya kijamii na kufanywa kwa kina kwenye mazao matatu ambayo yanalimwa na kuuzwa na wakulima wadogo ikiwemo mkonge, sukari na kahawa. Mazao haya yanazo sifa tofauti za kimimea, kilimo chake kina historia ndefu, vyombo vinavyoyashughulikia mazao haya vina miundo yake maalum na sifa zote hizi zinachangia mwenendo wa utendaji kwa sasa na vigezo mbali mbali vinavyoashiria matokeo ya ushindani kwenye masoko mbali mbali.

### Mbinu za utafiti

Utafiti ulichanganya mbinu kadha wa kadha za kiutafiti hususan uchunguzi wa kihistoria pamoja na mapitio ya maandishi, nyaraka kuu kuu na takwimu toka vyanzo mbali mbali. Mahojiano na watendaji wa serikali na wasio wa serikali pamoja na mawakala na wengineo wenye ujuzi kuhusu wakulima wadogo yalifanyika. Uchambuzi wa kihistoria na muktadha wa kitaalam uliomo kwenye kitabu unaonyesha kwa jinsi gani mfumo wa uzalishaji na muundo wa taasisi simamizi vinavyochangia kwenye matokeo ya ushindani kwenye masoko ya mazao nje na ndani ya nchi na unaonyesha pia kwamba katika vipindi vitatu kwenye historia ya nchi kuanzia uchumi wa mseto (1961-1967), kipindi cha ujamaa (1967-1985), hadi kipindi cha marekebisho ya kimuundo na mfumo wa kiuchumi tangu 1985 hadi sasa, mageuzi yaliyofanyika yakilenga ongezeko la tija na ushindani katika mazao ya kilimo kwenye masoko ya dunia yameathiriwa na vikwazo kadha wa kadha.

### Mabadiliko bunifu na uingizwaji wa wakulima kwenye sekta kadhaa

Kwenye sekta ndogo ya kahawa, wakati uzalishaji na soko la kahawa duniani

likipitia kwenye mabadiliko makubwa, Tanzania ilipoteza nafasi ya kujikita kwenye sehemu ya kimkakati ambako ingejiongezea nguvu ya ushindani kwenye soko la dunia. Hili lilichangiwa na chimbuko la sera ambazo zilivunja vyombo na mfumo muhimu kwenye uzalishaji, uandaaji na mauzo ya kahawa bora kwenye masoko ya kimataifa.

Kwenye sekta ndogo ya mkonge uingizwaji wa wakulima wadogo kwenye ubia na makampuni ya watu binafsi haukuleta mabadiliko ya kimsingi kwa wakulima wadogo kwa sababu ubia huo haukujengwa kwenye mahusiano yaliyozingatia usawa wa washiriki. Makampuni yalimiliki zana zote za uzalishaji zikiwemo ardhi, mitambo ya uchakataji, na taratibu za mauzo. Kwa vile taasisi za serikali hazikutaka kuingilia mahusiano hayo, ubia ule haukusaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya mkonge na ushindani kwenye soko.

Kwenye sekta ndogo ya sukari, kulikuwa na taasisi za kati ambazo zilisaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kuwaunganisha wakulima na masoko hodhi ya miwa. Pamoja na uzalishaji wa sukari kuongezeka Kilombero, uzalishaji wa wakulima wadogo haukuongezeka kwa kiasi kilichotarajiwa, na kwa upande wa Mtibwa kilianguka. Hii ni kwa sababu ya kutokuwepo uwiano mzuri kati ya wakulima wa miwa na viwanda vya sukari, na wakulima kupoteza uwezo wa kuwa na nguvu za pamoja. Ushahidi utaokanao na uchnguzi kwenye sekta hizi ndogo tatu unadhihirisha kwamba ili kuongeza tija kwenye uzalishaji na nguvu ya ushindani kwenye masoko, lazima kuwe na mikakati inayolenga kuweka uwiano katika ya wakulima wadogo na viwanda, kwa kutumia ubunifu na uratibu wa pamoja kati ya taasisi za dola na za kimasoko ili kupunguza vikwazo kwenye kila sekta ndogo husika.

## Masoko finyu ya karadha na ukosefu wa mikopo kwa wakulima

Ufinyu wa soko la karadha na ukosefu wa huduma za mikopo vijijini uliathiri sana jitihada za kuogeza uzalishaji kwa sababu bila ya uwezekano wa kupata mikopo wakulima wadogo walishindwa kujipatia nyenzo mpya za kiteknolojia ambazo zingewaongezea tija na pato.

## Matokeo ya sera za ujamaa

Sera za Ujamaa zilitegemea sekta ya umma peke yake katika kujenga uchumi na matokeo yake yakawa kudumaa kwa uchumi kati ya mwaka 1967 na 1985 na hii ilileta matatizo ya kiuchumi yaliyoambatana na upungufu mkubwa wa bidhaa muhimu, huduma duni kutoka kwenye mashirika ya umma, uzalishaji hafifu kwenye kilimo na viwanda, upungufu wa fedha serikalini na mapungufu kwenye urari wa malipo. Kwa sababu ya mashirika ya umma kuhodhi mamlaka ya kusambaza pembejeo na manunzi ya mazao, huduma hafifu zilipunguza uzalishaji na mapato ya wakulima kwa kiasi kikubwa.

## Sera za mabadiliko ya muundo

Sera hizi zilikuwa na lengo la kuimarisha nguvu za soko na kupunguza nafasi ya seikali katika kuendesha uchumi. Ingawaje zilisaidia kuleta marekebisho kwenye maeneo ya thamani ya fedha na utandawazi ulipanua wigo wa soko la karadha kwa wakulima, mabadiliko hayo hayo yalileta matatizo mapya, kwa mfano kushuka kwa kiwango cha mapato halisi ya wakulima, kuodolewa kwa ruzuku ya pembejeo na ongezeko la wasi wasi miongoni mwa watu maskini na wakulima kuhusu hatima yao. Matokeo ya haya yote ni kwamba ongezeko la ushindani na mauzo kwenye masoko ya nje halikulingana na matarajio ya wengi.

## Mageuzi kwenye bodi za mazao na kuyumba kwa mfumo wa kitaasisi

Mageuzi ya mfumo yaliambatana na mabadiliko ya muundo wa bodi za mazao ambazo zilipewa mamlaka ya kudhibiti bei za mazao, kusambaza pembejeo, pamoja na kuratibu na kutoa vibali kwa watu binafsi kununua mazao toka kwa wakulima. Ili kutekeleza majukumu yake, bodi hizi ziliweka viwango vya juu vya kodi na tozo kwenye mazao. Pia vyama vya ushirika viliwaona wanunuzi binafsi kama maadui wao na kuwazuia kununua mazao bila kupitia vyama vya ushirika.

## Usugu wa uzalishaji wa kujikimu katika sekta ya kilimo

Mageuzi kwa ujumla hayakuibadili sekta ya kilimo. Kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 1 sehemu kubwa ya mazao ya kilimo yaliendelea kuzalishwa kwa matumzi ya kujikimu na ni asilimia 14% tu ya mazao ilikuwa kwa ajili ya mauzo ya nje. Wakulima wadogo walizalisha 92% ya mazao yote ya kilimo na karibu nusu ya mauzo ya nje ya nchi yalizalishwa na wakulima wadogo. Ni kiasi kidogo cha mazao yote yalizalishwa kwenye mashamba madogo na makubwa.

### Jedwali 1: Mfumo jamii wa mazao ya kilimo 1992


| Aina ya uzalishaji | Matumizi ya kujikimu | | Mauzo nje | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | Bila mauzo | Mauzo | | |
| Wakulima wadogo | 51.00% | 34.10% | 6.40% | 91.6% |
| Mashamba makubwa | | 0.90% | 7.50% | 8.40% |
| Jumla | 51.00% | 35.00% | 14.00% | 100% |

***Chanzo:*** O'Laughlin (2004: 4)

## Kushuka kwa mchango wa mazao ya biashara kwa mauzo ya nje

Ingawaje kutokana na mageuzi yaliyoonyeshwa hapo juu, mchango wa mazao ya kilimo kwenye mauzo ya nje ulitegemewa kuongezeka, kihalisia ulishuka. Pia mchango wa mazao ya kawaida ambayo Tanzania iliyategemea kwa muda mrefu ulishuka kati ya 1961 na 2015 kama inavyoonyeshwa kwenye grafu namba 1 hapo chini.

***Grafu Namba 1: Mchango wa mazao sita makuu kwenye mauzo ya nje* 1961-2015**





***Chanzo: Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania*** (1983: 286-87); na Taarifa za Jamuhri ya Muungano wa Tanzania , Ripoti ya Hali ya uchumi (1989, 1995, 2002, 2005, 2008, 2010), Benki Kuu ya Taznania 2016.

## Mwenendo wa uzalishaji wa mazao makuu ya mauzo nchi za nje

Kwenye kitabu imeonyeshwa jinsi gani kulikuwa na kushuka kwa uzalishaji kwenye mazao muhimu sita: pamba, korosho, kahawa, katani, chai na tumbaku. Fahirisi ya kiwango cha mauzo nchi za nje kwa mazao haya kilichoko kwenye grafu Namba 2 hapo chini, kinaonyesha kwamba kati ya maika ya 1980 na 1990 kiwango cha mauzo kilishuka sana na kuongezeka kidogo miaka ya 1990 na kuendelea.

**Grafu Na. 2: Kielezo cha mauzo ya mazao makuu nje ya nchi 1960-2008 (-msingi 2006)**





**Chanzo:** *Wuyts 2008; Benki Kuu ya Tanzania (1983), Tathmini ya Utendaji wa Kisiasa na Kiuchumi (1961-1981); na Ripoti za Hali ya Uchumi 2007, 2008, and 2009.*

## Kudhoofika kwa taasisi za kati

Kushuka kwa viwango vya uzalishaji na ubora wa mazao kama kahawa kulichangiwa na hali ya kudhoofika kwa taasisi za kati hususan vyama vikuu vya ushirika na vyama vya ushirika vya msingi. Mabadiliko kwenye taasisi hizi yalivunja taratibu za uzalishaji na usimamizi kwenye mashina na kusababisha kuporomoka kwa ubora na uzalishaji wa mazao yote yaliyokuwa yanasimamiwa na vyombo hivi. Mifano ya mwenendo huu inaonyeshwa kwenye grafu Na 3 hapo chini.

**Grafu Na. 3: Mwelekeo kwenye uzalishaji wa kahawa 1951-2015 (kwa tani)**




***Chanzo:* Tanzania Ripoti za Takwimu 1951-1994, The Economic Surveys 1999, 2000, 2002, 2004, 2006, 2009, 2012, 2016**

## Ulinganisho wa mauzo nje na uagizaji toka nje

Kwa kipindi kirefu miaka ya 1960, ziada iliyokuwa inatokana na biashara na nchi za nje ilikuwa juu sana na kati miaka ya 1970 na 1980 mauzo na uagizaji nchi za nje vilishuka sana. Isitoshe tangia miaka ya 1970 kiwango cha gharama ya bidhaa zilizoagizwa toka nchi za nje ilikuwa juu zaidi kuliko mapato yaliyotokana na mauzo nchi za nje na kiwango cha tofauti kilizidi kupanda hadi katikati ya muongo wa 1990-2000. Baada ya mwaka 2000 mapato yaliyotokana na mauzo nchi za nje yalianza kupanda lakini pia gharama ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ilipanda na kushuka kwa kiwango kikubwa baada ya mwaka 2016 wakati bidhaa za kutoka nje zilipungua. Grafu Na. 4 inaonyesha mabadiliko haya tangu mwaka 1961.

**Grafu Na. 4: Asilimia ya mchango wa mauzo nje na bidhaa toka nje kwa pato la taifa 1961-2016**




***Chanzo:*** Ofisi ya Takwimu, Ofisi ya Rais-Tume ya Mipango (1991): Ripoti za Hali ya Uchumi (1995, 2002, 2007, 2010)

## Hitimisho

Kutokana na utafiti uliofanyika, imeonyeshwa dhahiri kwamba kiasi kikubwa cha mazao makuu na muhimu nchini bado kinazalishwa na wakulima wadogo na kwamba ili kuhakikisha kwamba uzalishaji, tija na mchango wa sekta ya kilimo kwa pato la taifa unaongezeka kwa kasi kikubwa, yafuatayo yangefaa kuzingatiwa. Kwanza ni kuongeza uwiano kati ya sekta binafsi na sekta ya uma. Pili kuna haja ya kupunguza gharama za

usimamizi zinazoingia kwenye bodi za mazao na vyama vya ushirika kwa sababu gharama hizi zinakinzana na lengo la kuongeza ufanisi kwenye utendaji na pato kwa wakulima. Tatu, mabadiliko yatafanikiwa ikiwa vyombo vya wakulima wenyewe vitaboreshwa na kufanywa ulingo wa kuleta na kutekeleza mabadiliko na mwisho, mabadiliko hayawezi kuleta mafanikio ya kutosha kama yanatilia mkazo zaidi mchakato wa usimamizi na kutotilia maanani matokeo ya usimamizi.

## Mapendekezo

Kufuatia matokeo ya utafiti inapendekezwa kwa Serikali:

***Kuzipitia upya sera zilizoko na za zamani*** na kuangalia mahali gani zimefanikiwa na wapi zinapwaya ili kupanga mikakati ya kuongeza tija na uwezo wa ushindani kwa kuondoa vikwazo vitakavyobainika.

***Kuviunda upya vyama vya wakulima*** kwa kiviongezea uwezo wakujisimamia na kuwapa wakulima nafasi ya kushiriki katika maamuzi yanayohusu uongozi, usambazaji wa nyenzo na pembejeo, mikataba, tozo na kodi na mikopo.

***Kutathmini mfumo na mchango wa bodi za mazao*** kwenye kuongeza uzalishaji wa mazao na mapato kwa wakulima na pia kwenye kuongeza ufanisi kwenye utendaji wake kwa nia ya kupunguza gharama za usimamizi na uhodhi kwenye usambazaji wa pemebejeo na manunuzi ya mazao nchini na nje ya nchi.

***Kuhimiza na kutoa vivutio kwa sekta binafsi*** ili kuwafanya waongeze uwekezaji na ushiriki katika kilimo cha kisasa na kuwajengea mazingira ya ubia na ushirikiano kati yao, wakulima wadogo na taasisi za umma ili kusaidia sekta ya kilimo kukua kwa tija.

***Kuwawezesha wakulima kupata mikopo kwa urahisi zaidi bila kupitia vyombo vya kati*** ili kupunguza gharama za mikopo. Aidha, mfumo wa uzalishaji kwa kuunganisha vipande vya ardhi vya wakulima wadogo kunaweza kurahisisha upatikaji wa mikopo mikubwa kwa ajili wa uwekezaji muhimu kama wa umwagiliaji.

***Kurejea mfumo wa ununuzi na mauzo ya mazao na kubuni upya muundo*** utaosaidia ongezeko la tija kwa uzalishaji wa wakulima wadogo na mchango wa sekta ya kilimo kwa pato la taifa.

## Baadhi ya Marejeleo


O'Laughlin, B. (2004). How Poverty Works: Gender and the Market Divide", in B. O'Laughlin and M. Wuyts (eds.), Study Guide on Conceptualizing Poverty. The Hague: Institute of Social Studies.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (1993). Ripoti ya Hali ya Uchumi 1992. Tume ya Mipango. Dar es Salaam.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (1996). Ripoti ya Hali ya Uchumi 1995. Dar es Salaam.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (1997). Sheria ya Katani 1997. Sheria Na. 2 of 1997.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (1999). Ripoti ya Hali ya Uchumi 1998, Tume ya Mipango. Dar es Salaam.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (2000) Ripoti ya Hali ya Uchumi 1999, Tume ya Mipango. Dar es Salaam.

Wuyts, M. (2004). Macroeconomic policy and trade integration: Tanzania in the world economy. in S. Bromley, M. Mackintosh, W. Brown, and Wuyts (eds.), *Making the International: Economic Interdependence and Political Order*, pp. 331-378. London and Sterling: Pluto Press.



REPOA
157 Mgombani/REPOA Street, Regent Estate
P.O. Box 33223, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2700083, Cell: +255 75 409 1677 Fax +255 22 2705738
Website: www.repoa.or.tz Email: repoa@repoa.or.tz


**Kituo cha Taarifa na Maarifa, REPOA**
Kituo chetu cha Taarifa na Maarifa kinatoa mazingira mazuri kwa utafiti wa fasihi na vitabu / maandiko mbali mbali kwa haraka na kwa urahisi wa matumizi ya maarifa na taarifa. Imeunganishwa na wavuti (internet) kwa ajili ya matumizi ya maktaba ya mkondoni (online) kuwasaidia wanaosomea Shahada za Uzamili na Uzamivu, watafiti na wasomi kwa kuwapatia magazeti, vitabu, ripoti n.k. ya siku za karibuni.

**Saa za Ufunguzi**
Kituo cha Taarifa na Maarifa kinakuwa wazi kuanzia Jumanne hadi Ijumaa saa 4.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana, saa 8.00 mchana hadi saa 11.00 alasiri. Maktaba ya mkondoni (online) ni wazi saa 24 kila siku.


@REPOA 2019
Matokeo, tafsiri, hitimisho, na maoni yaliyotolewa humu ndani ni ya mwandishi na siyo lazima yawe yanaakisi maoni na sera za REPOA.